The Tanganyika Law Society

The Bar Association Of Tanzania Mainland

26 Novemba, 2026.

TAMKO KUHUSU HUKUMU YA TUNDU ANTIPAS LISSU.

Tanganyika Law Society (TLS) imepokea kwa mitazamo na hisia mbalimbali hukumu iliyotolewa tarehe 6 Novemba 2026 dhidi ya Mwenyekiti wa CHADEMA, Mhe. Tundu Antipas Lissu, ambaye ni mwanachama wa Chama chetu na Rais Mstaafu wa Chama hicho, kuhusiana na shtaka la uhaini ambalo hatimaye lilibadilishwa na kuwa kosa dogo la uchochezi.

TLS imeona umuhimu wa kupitia kwa kina mwenendo mzima wa shauri hilo pamoja na hukumu iliyotolewa, kufuatia sintofahamu kubwa na mjadala uliojitokeza ndani na nje ya nchi kuhusu mwenendo wa kesi hiyo na uamuzi wa Mahakama.

Aidha, tumelazimika kufanya tathmini hiyo kutokana na hatua ya Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, ambayo kwa muda mrefu imeonekana kutotoa kauli au kuchukua hatua za wazi kuhusu matukio mbalimbali yanayohusisha madai ya ukiukwaji wa haki za binadamu, ikiwemo matukio ya watu kutekwa; wananchi waliokuwa wakifuatilia mwenendo wa kesi ya Mhe. Lissu kupigwa na kujeruhiwa katika siku za mwanzo za kesi; Wakili Mahinyila kupigwa na kudhalilishwa na maafisa wa polisi ndani ya mazingira ya Mahakama; pamoja na kuwepo kwa vikwazo vilivyoathiri upatikanaji wa taarifa kwa mawakili kuhusu masuala yaliyokuwa yakiendelea mahakamani, kinyume na misingi ya uhuru wa kupata na kutoa taarifa inayolindwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyorekebishwa.

Katika mazingira hayo, uamuzi wa Tume hiyo kujitokeza na kutoa maoni iliyoyataja kuwa ya kutokuwa na upande wowote (*neutral*), lakini ambayo kwa namna fulani yanaonekana kuunga mkono sehemu ya hukumu iliyotolewa, pamoja na Mahakama kujitokeza kutetea uwepo wa nakala tofauti za hukumu moja umeongeza umuhimu wa kuwepo kwa tathmini huru, ya kitaalamu na yenye kuzingatia misingi ya sheria kuhusu shauri hilo.

Kama taasisi ya kitaaluma, ambayo kwa mujibu wa Kifungu cha 4 cha Sheria ya Chama cha Wanasheria Tanganyika (Tanganyika Law Society Act) ina wajibu wa kulinda maslahi ya wanachama wake, kutetea maslahi ya umma na kushiriki katika kukuza na kulinda utawala wa sheria, haki za binadamu, Katiba na misingi ya ukatiba (*constitutionalism*), TLS ina wajibu

wa kuzungumzia masuala yenye athari kwa utoaji wa haki na imani ya wananchi katika mfumo wa haki nchini. Aidha kwa kuwa TLS ni taasisi ya watanzania ina haki ya kushiriki katika maswala yanayogusa au kuathiri umma kwa mujibu wa ibara ya 21 ya Katiba ya JMT, 1977.

Kwa msingi huo, baada ya kupitia mwenendo wa shauri na sababu zilizotolewa na Mahakama katika kufikia uamuzi wake hasa kwa kuzingatia uchambuzi na ushauri wa wataalamu wetu, TLS imeona kuna umuhimu wa kutoa maoni na/ au tamko rasmi linalobainisha maeneo yenye mapungufu ya kisheria na kiutaratibu yanayohitaji kuangaliwa kwa kina.

Lengo la tamko hili si kuingilia uhuru wa Mahakama wala kupinga mamlaka yake ya kikatiba ya kutafsiri na kutumia sheria, bali ni kutekeleza wajibu wa kitaaluma wa kuhimiza uwajibikaji, kuimarisha misingi ya utoaji haki na kulinda imani ya wananchi katika Mahakama kama chombo muhimu na cha mwisho cha utoaji haki, kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

TLS inatambua kuwa yapo maeneo ambayo Mahakama ilionesha umakini katika kushughulikia shauri hilo. Maeneo hayo ni pamoja na uamuzi wa kuzuia uingizwaji wa ushahidi mpya ambao haukuwepo katika mwenendo wa awali wa shauri, kuondoa au kutokuzingatia baadhi ya video zilizowasilishwa na mchunguzi ambaye sifa zake za kitaaluma zilikuwa zinatiliwa mashaka, kurusha moja kwa moja mwenendo katika mahakama kabidhi Kisutu, pamoja na kufanya tathmini ya ushahidi na kufikia hitimisho kwamba hapakuwa na ushahidi wa kutosha kuthibitisha kosa la uhaini.

Hata hivyo, licha ya hatua hizo chanya, TLS inaamini kuwa bado kuna maeneo kadhaa yenye mapungufu makubwa ya kisheria na kiutaratibu ambayo yanahitaji kuchunguzwa na kufanyiwa kazi kwa umakini. Mapungufu hayo, yasipotambuliwa na kushughulikiwa ipasavyo, yanaweza kuwa na athari kubwa katika misingi ya utoaji haki, ulinzi wa haki za msingi za wananchi na, zaidi ya yote, kuathiri imani ya umma katika Mahakama na vyombo vingine vya usimamizi wa haki nchini.

Kwa hiyo, TLS inaona kuwa ni wajibu wake kuweka wazi hoja hizo kwa misingi ya sheria, ushahidi na kanuni za haki, kwa lengo la kuchochea mjadala wa kitaaluma na kuhimiza maboresho yanayohitajika katika mfumo wa utoaji haki nchini Tanzania.

1. MAPUNGUFU MAKUU YA KISHERIA KATIKA HUKUMU

Bila kuathiri heshima ya kitaasisi inayostahili Mahakama na Waheshimiwa Majaji, na kwa kutambua mamlaka na wajibu wao wa kikatiba katika kusimamia utoaji wa haki, TLS inaona kuwa hukumu hiyo ina maeneo kadhaa yenye mapungufu ya kisheria na kiutaratibu yanayohitaji kuangaliwa kwa kina. Mapungufu hayo ni pamoja na yafuatayo:

1.1 Kuminya Haki ya Kutoa Maoni na Uhuru wa Kujieleza

TLS inaona kuwa Mahakama haikufanya tathmini ya kutosha ya mpaka wa kikatiba na kisheria unaotenganisha ukosoaji wa kisiasa na kauli zinazoweza kustahili kuainishwa kama uchochezi. Aidha, zuio lililowekwa dhidi ya mawakili kutoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu mwenendo na masuala yanayojitokeza katika shauri hilo linaibua maswali mazito kuhusu uzingatiaji wa haki ya kupata na kutoa taarifa inayolindwa na Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sheria za habari pamoja na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania ni sehemu yake.

Jambo hili linapaswa kutazamwa kwa upana zaidi, kwa kuzingatia hatua ambazo Mahakama za Tanzania zilikuwa zimepiga katika kukuza uwazi wa shughuli za utoaji haki. Kwa mfano, katika hatua za awali za shauri hilo, Mahakama iliruhusu matangazo ya moja kwa moja ya mwenendo wa kesi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu. Hata hivyo, katika hatua za mwisho za shauri, Mahakama iliamua kusitisha matangazo hayo bila kutoa sababu za wazi za uamuzi huo. Mabadiliko hayo yanaibua hoja muhimu kuhusu misingi iliyotumika katika kuamua kiwango cha uwazi kilichopaswa kutumika katika shauri hilo.

TLS inasisitiza kuwa uwazi katika utoaji haki si jambo la hiari au la mapambo ya kimahakama, bali ni moja ya misingi muhimu ya utawala wa sheria, uwajibikaji na ujenzi wa imani ya wananchi kwa Mahakama hasa kwa vile mamlaka ya nchi ikiwemo mhimili wa mahakama yanatoka kwa wananchi. Katika mifumo ya kidemokrasia, uwazi unazidi kutambuliwa kama nyenzo muhimu ya kuhakikisha wananchi wanapata fursa ya kuelewa na kufuatilia namna haki inavyotendeka. Hali hiyo inajidhihirisha pia katika mifumo ya kikanda na kimataifa.

Kwa mfano, nchini Kenya, uwazi katika shughuli za Mahakama umepewa nafasi kubwa, si katika uendeshaji wa mashauri pekee, bali pia katika baadhi ya michakato ya kitaasisi, ikiwemo ushiriki wa umma katika michakato ya uteuzi wa majaji na shughuli za Tume ya Utumishi wa Mahakama.

Katika mazingira haya, TLS inaona kuwa ni muhimu Mahakama kuweka wazi sababu za msingi za kusitisha matangazo ya moja kwa moja ya mwenendo wa shauri hilo, ili kuondoa mashaka yanayoweza kujitokeza miongoni mwa wananchi. Bila ufafanuzi wa kutosha, hatua

hiyo inaweza kuibua hisia kwamba uwazi ulipunguzwa katika shauri lililokuwa na maslahi makubwa kwa umma. Swali la msingi linalostahili kujibiwa ni: ni sababu zipi za kisheria na kiutendaji zilizohalalisha kupunguza kiwango cha uwazi katika shauri hilo, na hatua hiyo ililenga kulinda maslahi gani?

1.2. Mapungufu katika Tathmini na Uchambuzi wa Ushahidi

TLS inatambua na kuheshimu mamlaka ya Mahakama ya kupokea, kuchambua, kupima na kutoa uzito kwa ushahidi unaowasilishwa na pande zinazohusika katika shauri. Hata hivyo, heshima hiyo haiondoi wajibu wa kitaaluma wa kuchunguza kama misingi ya kisheria inayosimamia upokeaji na tathmini ya ushahidi ilizingatiwa ipasavyo katika kufikia uamuzi.

Kwa tathmini ya TLS, kuna maeneo yanayoibua maswali kuhusu namna kanuni za sheria ya ushahidi zilivyotumika, hususan baada ya shtaka la awali la uhaini kubadilishwa na kuwa kosa la uchochezi. Mabadiliko hayo yalihitaji tathmini mahsusi ya viashiria vya kisheria vya kosa jipya, vipengele vyake na ushahidi uliotakiwa kuthibitisha kila kipengele cha kosa hilo.

Kwa namna hukumu ilivyojengwa na hoja zilivyochambuliwa, kuna mazingira yanayoweza kutoa taswira kwamba mzigo wa kuthibitisha kutokuwa na hatia ulihamishiwa kwa mshtakiwa, badala ya kubaki kwa upande wa Jamhuri ambao ndio wenye wajibu wa kuthibitisha mashtaka dhidi yake. Mwelekeo huo, iwapo utathibitishwa, unakinzana na msingi wa kikatiba wa dhana ya kutokuwa na hatia (*presumption of innocence*), ambao unamtaka mshtakiwa kuchukuliwa kuwa hana hatia mpaka ithibitishwe vinginevyo kwa mujibu wa sheria.

Aidha, uchambuzi wa hukumu unaibua wasiwasi kwamba uzito mkubwa uliwekwa katika kuangalia mapungufu madogo madogo ya utetezi, badala ya kujikita kwa kina katika kupima ubora, uthabiti, uaminifu na uzito wa ushahidi uliowasilishwa na upande wa mashtaka. Ni muhimu kukumbuka kuwa wajibu wa msingi wa kuthibitisha mashtaka unabaki kwa upande wa Jamhuri, na si kwa mshtakiwa kujithibitisha kuwa hana hatia.

TLS inaamini kuwa katika mashauri ya jinai, na hasa yale yenye uzito mkubwa kwa haki na uhuru wa msingi wa mtu, tathmini ya ushahidi inapaswa kuongozwa na misingi ya haki ya kusikilizwa, dhana ya kutokuwa na hatia na wajibu wa upande wa mashtaka kuthibitisha kila kipengele cha kosa kwa kiwango kinachotakiwa na sheria. Kupotoka katika misingi hiyo kunaweza kuathiri haki ya mshtakiwa na uadilifu wa mchakato mzima wa utoaji haki.

2. MASWALI YENYE UTATA NA HOJA ZA MSINGI ZA KISHERIA ZINAZOHITAJI UFAFANUZI

Kufuatia uchambuzi wa mwenendo wa shauri na hukumu iliyotolewa, Tanganyika Law Society (TLS) inaibua maswali kadhaa ya msingi yenye utata wa kisheria na kiutaratibu ambayo, kwa mtazamo wetu, yanahitaji ufafanuzi wa kina kutoka kwa Mahakama na wadau wengine wa mfumo wa utoaji haki. Maswali haya yanatokana na umuhimu wa kulinda haki ya kusikilizwa kwa haki (*right to a fair hearing*), uhuru wa Mahakama, uadilifu wa mwenendo wa mashauri na imani ya wananchi katika mfumo wa utoaji haki.

Maswali hayo ni yafuatayo:

1. Kuhusu muundo wa jopo la majaji

Ni kwa msingi gani wa kisheria na kiutaratibu Jaji Mkuu aliamua shauri la uhaini lililomhusu Mhe. Tundu Lissu lisikilizwe na jopo la majaji watatu badala ya Jaji mmoja, kama ilivyokuwa katika mashauri mengine ya aina hiyo? Je, uamuzi huo ulizingatia vigezo gani vya kisheria, na ni kwa namna gani ulilingana na misingi ya usawa katika usimamizi wa mashauri ya jinai?

2. Kuhusu matumizi ya mashahidi wa kificho

Ni kwa kiwango gani haki ya mshtakiwa ya kusikilizwa kwa haki (*right to a fair hearing*) inalindwa pale ambapo upande wa mashtaka unatumia mashahidi wa kificho ambao utambulisho wao hauwekwi wazi kwa utetezi? Ni hatua zipi za kisheria zinazochukuliwa kuhakikisha kuwa matumizi ya mashahidi hao hayaathiri haki ya mshtakiwa kuhoji ushahidi unaotolewa dhidi yake?

3. Kuhusu usiri katika maombi ya kuficha utambulisho wa mashahidi

Mchakato wa kusikiliza maombi ya upande wa mashtaka ya kuficha utambulisho wa mashahidi kwa usiri unalindaje haki za msingi za mshtakiwa? Ni kwa namna gani Mahakama inahakikisha kuwa maamuzi ya aina hiyo hayazuii utetezi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kupinga hoja na ushahidi unaowasilishwa?

4. Kuhusu usajili wa majina ya mashahidi wa utetezi

Ni kwa nini Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, ilikataa kuandika au kurekodi majina ya mashahidi waliopendekezwa na mshtakiwa, licha ya wajibu wa

Mahakama kusimamia haki ya kila upande kuwasilisha mashahidi wake kwa mujibu wa sheria? Ni msingi gani wa kisheria uliotumika kufikia uamuzi huo?

5. Kuhusu kunyimwa fursa ya kuita mashahidi wa utetezi

Ni kwa nini Mhe. Tundu Lissu alizuiwa kuita baadhi ya mashahidi aliowapendekeza, wakiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan; Makamu wa Rais wa wakati huo, Mhe. Philip Mpango; Waziri Mkuu wa wakati huo, Mhe. Kassim Majaliwa; na Mkuu wa Usalama wa Taifa?

Je, Mahakama ilitumia vigezo gani kuhitimisha mapema kuwa mashahidi hao hawakuwa na uhusiano na shauri hilo kabla ya kusikiliza ushahidi ambao wangetarajiwa kuutoa? Kwa kuwa umuhimu na uhusiano wa shahidi na shauri unaweza kutathminiwa pia kutokana na maelezo na ushahidi anaotarajiwa kutoa, je, uamuzi huo haukuingilia haki ya mshtakiwa kuwasilisha utetezi wake kikamilifu?

6. Kuhusu utetezi wa nia ya kutenda kosa la uchochezi

Ni katika hatua gani ya mwenendo wa shauri Mhe. Tundu Lissu alipewa fursa ya kujitetea mahususi kuhusu kiini cha nia (*criminal intent*) ya kutenda kosa la uchochezi? Je, Mahakama ilifanya tathmini ya kutosha kuhusu uwepo wa nia hiyo kwa kuzingatia vipengele vya kisheria vya kosa husika?

7. Kuhusu taarifa ya kosa jipya (Notice of the New Charge)

Ni lini na kwa utaratibu gani Mahakama ilimtaarifu mshtakiwa kuhusu uwezekano wa kuwajibishwa kwa kosa jingine tofauti na shtaka la awali la uhaini? Je, taarifa hiyo ilitolewa kwa wakati na kwa namna iliyomwezesha mshtakiwa kuelewa tuhuma mpya, kujiandaa na kutoa utetezi wake kikamilifu bila kuathiri haki yake ya kusikilizwa kwa haki?

8. Kuhusu uhusiano wa kisheria kati ya uhaini na uchochezi

Je, kwa mujibu wa sheria ya jinai, kosa la uhaini lina kosa dogo (*lesser offence*) linaloweza kutolewa kama mbadala wa hatia ya kosa hilo? Ikiwa jibu ni ndiyo, je, uchochezi unaweza kisheria kuchukuliwa kuwa kosa dogo la uhaini, ilhali makosa hayo yana viini na vipengele tofauti vya kisheria?

9. Kuhusu viini vya makosa ya uhaini na uchochezi

Je, viini vya kosa (*ingredients of the offence*) vya uhaini vinafanana na viini vya kosa la uchochezi? Ikiwa makosa hayo yana vipengele tofauti vya kisheria, ni kwa msingi gani

Mahakama iliweza kubadilisha shtaka la awali na kutoa hatia kwa kosa jingine bila kuathiri haki ya mshtakiwa kujua na kujibu tuhuma mahsusi zilizokuwa mbele yake?

10. Kuhusu haki ya kuwasiliana na mawakili na kujiandaa kwa utetezi

Katika shauri la kikatiba lililofunguliwa na mawakili kuhusu haki za wafungwa kukutana na kupata ushauri wa kisheria kutoka kwa mawakili wao, ilibainishwa kuwa Mhe. Lissu alikosa fursa ya kutumia kikamilifu haki yake ya kusikilizwa na kujiandaa kwa utetezi. Kwa nini Mahakama haikuzingatia matokeo na athari za ukiukwaji huo katika kutathmini uhalali wa mwenendo wa shauri, wakati wa kutoa hukumu na hata wakati wa kuamua adhabu?

11. Kuhusu hali ya kiafya na muda aliokaa gerezani

Ni kwa nini Mahakama, wakati wa kutoa adhabu, haikuzingatia kwa uzito unaostahili hali ya kiafya ya Mhe. Tundu Lissu? Aidha, ni kwa nini siku 577 alizokuwa amekaa kizuizini hazikuonekana kupunguzwa katika adhabu iliyotolewa dhidi yake? Je, Mahakama ilizingatia vigezo vyote vya kisheria na kibinadamu vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kutoa adhabu?

12. Kuhusu msingi wa kuchagua kifungo badala ya faini

Ni kwa kiwango gani hoja zilizotolewa kuhalalisha adhabu ya kifungo badala ya faini kwa kosa lililohukumiwa zina msingi wa kisheria, kimantiki na kiushahidi? Je, Mahakama ilizingatia kwa uwiano unaostahili uzito wa kosa, mazingira ya mtuhumiwa, madhumuni ya adhabu na uwezekano wa kutumia adhabu mbadala?

13. Kuhusu muda na mchakato wa kufikia makubaliano ya adhabu

Ni muda gani jopo la majaji lilitumia kujadili na kufikia makubaliano kuhusu aina na kiwango cha adhabu kilichopaswa kutolewa? Swali hili linaibuliwa kutokana na namna adhabu ilivyotangazwa na mwenyekiti wa jopo mara tu baada ya mshtakiwa kupewa fursa ya kusema kuhusu adhabu. Je, utaratibu huo unaonesha kuwa tathmini ya kina ya mazingira ya mshtakiwa na hoja za pande zote ilifanyika kabla ya adhabu kutangazwa?

14. Kuhusu matumizi ya kifungu cha kosa dogo

Ni kwa nini Mahakama iliamua kutafuta na kutumia kosa dogo lililopo katika kifungu cha mwisho cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, wakati hata upande wa Jamhuri haukuwa

umeomba Mahakama ichukue hatua hiyo? Je, Mahakama ilizingatia athari za kisheria na kiutaratibu za kutumia mamlaka hayo katika mazingira ya shauri husika?

Aidha, hatua hiyo inaibua swali muhimu kuhusu mipaka ya mamlaka ya Mahakama katika kutafuta na kubadilisha msingi wa hatia ambao haukuombwa na upande wa mashtaka. Je, hatua hiyo inaweza kuibua taswira ya Mahakama kujitwika jukumu la upande wa mashtaka, na kwa namna gani hali hiyo inaathiri mtazamo wa umma kuhusu uhuru, kutopendelea upande wowote na uadilifu wa Mahakama, hasa ikizingatiwa kuwa Mhe. Tundu Lissu mwenyewe aliibua hoja kuhusu suala hilo wakati wa kutolewa kwa hukumu?

15. Kuhusu matumizi ya taarifa na matukio ambayo hayakuwa sehemu ya ushahidi

Ni kwa nini Mahakama, wakati wa kutoa adhabu, ilizingatia taarifa na matukio ambayo hayakuwasilishwa kama ushahidi rasmi mahakamani na ambayo mshtakiwa hakupata fursa ya kuyapinga au kujitetea dhidi yake? Mfano ni matumizi ya Ripoti ya Jaji Chande na matukio ya vurugu za tarehe 29 Oktoba 2025, ambayo kwa mujibu wa mwenendo wa shauri hayakuwa yamewasilishwa kama ushahidi wa kuthibitisha tuhuma dhidi ya mshtakiwa.

Je, matumizi ya taarifa hizo katika hatua ya kutoa adhabu hayakukiuka haki ya mshtakiwa kujua ushahidi unaotumika dhidi yake na kupata fursa ya kuupinga kabla ya Mahakama kuufanyia kazi?

16. Kuhusu uhusiano wa kisababishi na ukaribu wa muda (Proximity)

Ikiwa madai ya uchochezi yanahusishwa na matamshi yaliyotolewa mwezi Aprili 2025, na matukio ya vurugu yanadaiwa kutokea tarehe 29 Oktoba 2025, Mahakama ilitumia vigezo gani vya kisheria na kiushahidi kuthibitisha uhusiano wa moja kwa moja wa kisababishi kati ya matamshi hayo na matukio yaliyotokea takribani miezi sita baadaye?

Je, Mahakama ilichunguza kwa kina suala la ukaribu wa muda (*temporal proximity*), mazingira mengine yaliyoweza kuchangia kutokea kwa matukio hayo na uwepo wa ushahidi unaothibitisha kuwa matamshi ya mshtakiwa ndiyo yaliyosababisha matukio hayo?

17. Kuhusu uaminifu na uthibitisho wa mashahidi wa kificho

Ni kwa nini Mahakama iliamua kutegemea ushahidi wa mashahidi ambao walikuwa wamekamatwa na baadaye kuachiwa huru ili kutoa ushahidi wa kificho? Ni tathmini gani ilifanyika kuhusu mazingira ya kukamatwa na kuachiwa kwao, uwezekano wa kuwa na maslahi binafsi katika shauri na uaminifu wa ushahidi wao?

Aidha, kwa nini ushahidi huo haukuungwa mkono na ushahidi mwingine huru na wa kuaminika (*independent corroborative evidence*) ili kuimarisha uthibitisho wa madai yaliyotolewa dhidi ya mshtakiwa?

18. Kuhusu mipaka kati ya ukosoaji wa kisiasa na uchochezi

Je, matamshi ya kisiasa yanayotolewa na kiongozi wa chama cha upinzani kwa lengo la kukosoa sera, maamuzi au vitendo vya Serikali na viongozi wake yanapaswa kuchukuliwa moja kwa moja kuwa ni uchochezi na uvunjifu wa amani, au yanapaswa kutazamwa kama sehemu ya uwajibikaji wa kidemokrasia na utekelezaji wa haki ya kikatiba ya kutoa maoni?

Ni kwa vigezo gani vya kisheria vinavyotofautisha ukosoaji halali wa kisiasa na uchochezi vinavyopaswa kutumika katika kufanya tathmini hiyo?

19. Kuhusu tafsiri ya kosa la uchochezi na athari zake kwa demokrasia

Ni kwa namna gani Mahakama ilitafsiri na kupima maana ya neno na kosa la uchochezi bila kuweka mazingira yanayoweza kuleta athari ya kuwatisha au kuwakatisha tamaa viongozi wa vyama vya siasa na wananchi wengine kutekeleza wajibu wao wa kikatiba wa kuikosoa Serikali?

Je, tafsiri iliyotumika inazingatia mizania inayotakiwa kati ya kulinda amani na usalama wa umma, kwa upande mmoja, na kulinda uhuru wa kujieleza, ushindani wa kisiasa na demokrasia, kwa upande mwingine?

20. Kuhusu uchaguzi wa njia na sheria za kisheria za kushughulikia matamshi husika

Ikiwa matamshi yaliyotolewa na Mhe. Tundu Lissu yalikuwa na athari za kisheria katika eneo la madai (*civil liability*), ni kwa nini njia za kisheria za madai hazikuzingatiwa kabla ya kuanzishwa kwa hatua za jinai, iwapo sheria husika ziliruhusu njia hiyo?

Aidha, kwa kuwa matamshi yanayohusika yalichapishwa kupitia mtandao wa YouTube wa Jambo TV, ni kwa nini upande wa mashtaka haukuzingatia uwezekano wa kutumia mfumo wa sheria na kanuni zinazosimamia maudhui ya mtandaoni (*Online Content Regulations*), iwapo yalikuwa na masharti yanayohusika na madai hayo? Je, uchaguzi wa njia ya kisheria iliyotumika ulizingatia kwa usahihi aina ya kosa linalodaiwa na mazingira ya tukio?

21. Kuhusu uwepo wa hukumu tatu tofauti na uadilifu wa kumbukumbu za Mahakama

Ni kwa nini shauri la Mhe. Tundu Lissu limekuwa na matoleo au kumbukumbu tatu tofauti za hukumu? Tofauti hizo zinaelezeka vipi kwa kuzingatia taratibu za uandishi, uhakiki, uidhinishaji na utunzaji wa kumbukumbu rasmi za Mahakama?

Je, tofauti hizo zina athari gani katika misingi ya uadilifu wa kumbukumbu na mwenendo wa Mahakama (*integrity of court records and proceedings*), uhakika wa kisheria na imani ya mwananchi wa kawaida katika mfumo wa utoaji haki?

TLS inaona kuwa maswali haya si ya kupuuzwa wala kuchukuliwa kama mashambulizi dhidi ya Mahakama au Waheshimiwa Majaji. Ni hoja za kitaaluma zinazotokana na wajibu wa kikatiba na kitaasisi wa kuhakikisha kuwa sheria inatafsiriwa na kutumika kwa usahihi, haki za msingi zinalindwa na taratibu za utoaji haki zinakuwa wazi, thabiti na zinazoweza kuaminika.

Kwa msingi huo, TLS inahimiza maswali haya yajibiwe kwa hoja za kisheria, ushahidi na misingi ya haki, kwa kuwa imani ya wananchi katika Mahakama haijengwi kwa kutokuwepo kwa ukosoaji, bali kwa uwezo wa Mahakama kutoa maamuzi yenye misingi imara ya kisheria, yanayoweza kuchunguzwa kitaaluma na kustahimili tathmini ya umma.

3. WITO KWA WADAU NA MAMLAKA HUSIKA

Kwa kuzingatia hoja na mapungufu yaliyoainishwa katika tamko hili, Tanganyika Law Society (TLS) inatoa wito kwa wadau na mamlaka mbalimbali kuchukua hatua zifuatazo:

1. Kwa Timu ya Mawakili wa Utetezi, ikiwemo Mawakili kutoka TLS:

TLS inaitaka Timu ya Mawakili wa Utetezi, kwa kushirikiana na mawakili watakaotolewa na TLS, kuchukua hatua stahiki na za haraka za kisheria, ikiwemo kukata rufaa katika Mahakama ya Rufani ya Tanzania, ili kuwezesha uchunguzi na tafsiri ya kina ya masuala ya kisheria yaliyojitokeza katika hukumu hiyo na hatimaye kuhakikisha haki inatendeka.

Aidha, TLS inasisitiza umuhimu wa kuchukua hatua zote halali na zinazowezekana kisheria kuhakikisha kuwa afya, usalama na uhuru wa Mhe. Tundu Lissu vinalindwa wakati taratibu za kisheria za kupinga uamuzi huo zikiendelea. Ulinzi wa haki zake za msingi unapaswa kupewa kipaumbele katika hatua zote za mchakato huo.

2. Kwa Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania:

TLS inatoa wito kwa Serikali na Bunge kuharakisha utekelezaji wa mapendekezo ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Mfumo wa Haki Jinai, kwa kutambua kuwa mapendekezo hayo yalibainisha changamoto mbalimbali za msingi katika mfumo wa haki jinai nchini.

Changamoto hizo ni pamoja na madai ya kubambikiwa kesi, uwepo wa vituo visivyo rasmi vya kuweka watu kizuizini, matumizi yasiyo sahihi ya makosa makubwa ya jinai kama vile uhaini na ugaidi, pamoja na matumizi ya makosa yasiyokuwa na dhamana kama nyenzo za kuwanyima watu uhuru na kuwaadhibu kabla hata ya kuthibitishwa kwa hatia zao.

TLS inasisitiza kuwa makosa makubwa ya jinai yanapaswa kutumika kwa kuzingatia ushahidi na masharti ya sheria, na si kama nyenzo ya vitisho, shinikizo au ukandamizaji wa haki na uhuru wa wananchi. Utekelezaji wa mapendekezo ya Tume hiyo ni hatua muhimu katika kujenga mfumo wa haki jinai unaozingatia haki za binadamu, uwajibikaji na utawala wa sheria.

3. Kwa Wananchi, Wanaharakati na Watetezi wa Haki za Binadamu:

TLS inatoa wito kwa wananchi, wanaharakati na watetezi wa haki za binadamu kutokata tamaa katika kusimamia misingi ya utawala bora, demokrasia, haki za binadamu na uwajibikaji wa viongozi wa umma. Wanapaswa kuendelea kutekeleza wajibu wao wa kiraia kwa kutumia njia za amani na taratibu zinazotambuliwa na sheria katika kutetea na kudai haki.

Aidha, TLS inawahimiza wananchi kuendelea kutoa elimu kwa viongozi na watendaji wa umma ambao wanaweza kuwa na mtazamo kwamba harakati za kudai haki, kukosoa mifumo ya uongozi au kupendekeza mabadiliko ya kijamii na kisiasa ni vitendo vya uhalifu. Mtazamo huo unahitaji kurekebishwa kwa kuzingatia historia ya taifa letu na misingi ya demokrasia.

Ni muhimu kukumbuka kuwa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Baba wa Taifa na mmoja wa waasisi wa taifa letu, alikuwa sehemu ya harakati za kudai uhuru, haki na kujitawala. Aidha, dhana ya uanaharakati haipaswi kufungamanishwa na maandamano au shughuli za kisiasa pekee. Hata juhudi za kitaasisi na kimahakama za kupinga mifumo kandamizi na kurekebisha sheria na vitendo vinavyokiuka haki za binadamu ni sehemu ya harakati pana za kutetea haki. Kwa mfano, maamuzi ya Mahakama yanayolenga kuzuia ndoa za utotoni ni kielelezo cha namna ambavyo mapambano ya haki yanaweza kuendelezwa kupitia mifumo ya kisheria na kitaasisi.

Kwa msingi huo, TLS inasisitiza kuwa uanaharakati unaozingatia sheria, unaolenga kulinda haki za binadamu na kuimarisha utawala wa sheria ni sehemu halali na muhimu ya maendeleo ya jamii ya kidemokrasia.

4. HITIMISHO

TLS inatoa wito kwa wanachama wake, wadau wa sheria na haki za binadamu, taasisi za umma, wananchi na wanaharakati kwa ujumla kuendelea kusimamia misingi ya haki, uwazi, uwajibikaji na utawala wa sheria.

Tunasisitiza kuwa **haki haiwezi kujengwa kwa kuwanyamazisha wanaotoa hoja au kuwakandamiza wakosoaji, bali kwa kusikiliza hoja zao, kuzitathmini kwa misingi ya sheria na kushughulikia changamoto wanazozibainisha.**

Vilevile, tunakumbusha kuwa haki si suala la maslahi ya mtu mmoja au kundi fulani, bali ni msingi mkuu wa amani, mshikamano, demokrasia na maendeleo endelevu ya taifa. Taifa lenye nguvu ni lile linalothubutu kukabiliana na mapungufu yake, kulinda haki za kila mmoja na kuhakikisha kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria.

Imetolewa na Baraza la Uongozi la Chama Cha Wanasheria Tanganyika (TLS).



BONIFACE A. K. MWABUKUSI
RAIS-TLS